

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAISI  
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA**

**SIMU YA UPEPO: "REGCOM "**

**SIMU NA:- 023-220-2098**

**FAX NA. 023-220-2502**

**Email: ras.lindi@tamisemi.go.tz**



**OFISI YA MKUU WA MKOA,  
S.L.P. 1054,  
LINDI.**

**07 Mei, 2021.**

**TARATIBU ZA USAJILI WA KAMPUNI ZA UNUNUZI WA ZAO LA  
UFUTA/MBAAZI MSIMU 2021**

Mkoa unawatangazia wanunuza wote wa zao la ufuta/mbaazi kuwa, Msimu wa ununuza wa zao la ufuta utaanza rasimi tarehe 29 Mei 2021. Mfumo utakaotumika ni stakabadhi ghalani, ambapo ufuta/mbaazi utakusanya kupitia vyama vya Msingi vya Ushirika na baadae kusafirishwa kwenda ghalaa kuu za minada. Ufuta huo utauzwa kupitia minada itakayofanyika kila siku ya Jumamosi na Jumapili ya wiki katika maeneo yanayolima mazao hayo.

Wanunuza wote wanatakiwa kujisajili Ofisi ya Mkoo wa Mkoa Lindi kabla ya kwenda kushiriki katika minada itakayofanyika. (**Hakuna kampuni itakayoruhusiwa kushiriki kwenye mnada bila kusajiliwa**)

Mambo muhimu yanayohitajika ili kampuni iweze kupata usajili ni;

- i. Nakala ya leseni hai ya biashara (Valid business licence)
- ii. Nakala ya cheti cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN/VAT certificate)
- iii. Nakala ya hati ya kutodaiwa kodi ya ndani ya nchi (Tax clearance)
- iv. Nakala ya cheti cha usajili wa kampuni (Certificate of incorporation /certificate of registration)
- v. Picha mbili za rangi za wakurugenzi wa kampuni
- vi. Taarifa za benki zisizopungua miezi mitatu (Bank statement)
- vii. Baada ya usajili mnunuzi atapewa maelekezo ya namna ya kushiriki kwenye minada kulingana na mwongozo wa zao la ufuta na mbaazi uliyopitishwa na wadau wa ufuta na mbaazi Mkoa wa Lindi.

NB: Utaratibu huu ndio utakaotumika msimu 2021 na usajili utaanza rasmi tarehe 11 Mei 2021.

Imeandaliwa na;  
Ofisi ya Mkoo wa Mkoa,  
S.L.P 1054  
**LINDI**